

## USHAURI SABA ZA KUZUNGUMZA NA MTOTO WAKO



- 1 Zungumza na mtoto wako kwa njia isiyo ya haraka, ukipumzika mara kwa mara.** Ngoja sekunde chache baada ya mtoto wako kumaliza kuongea kabla hujaanza kusema. Usemi wako mwenyewe wa polepole na mtulivu utakuwa wa umuhimu zaidi kuliko ukosoaji wowote au ushauri kama vile “ nenda polepole” au “ jaribu tena polepole.”
- 2 Punguza idadi ya maswali unayomuuliza mtoto wako.** Badala ya kuuliza maswali, toa maoni tu kuhusu alichosema mtoto wako, hivyo kumfanya ajue kuwa umemsikia. Watoto huzungumza kwa uhuru zaidi ikiwa wanaeleza mawazo yao wenyewe badala ya kujibu maswali ya mtu mzima.
- 3 Tumia ishara zako za usoni na lugha nyingine ya mwili kumtumia ujumbe mtoto wako kwamba unasikiliza kilicho kwenye ujumbe wake na sio jinsi anavyozungumza.**
- 4 Panga dakika chache za muda usiobadilika kila siku ambazo unaweza kumpa mtoto wako umakini usiokatizwa.** Unaposema wakati wa muda huu maalumu, tumia usemi wa polepole, mtulivu na mwepesi, wenye mapumziko ya kutosha. Muda huu mtulivu unaweza kuwa kijenga imani kwa watoto wadogo, ukiwaruhusu hujua kwamba unafurahia kuwa pamoja nao.
- 5 Saidia jamaa wote wa familia kujifunza kuchukua zamu kwa kuzungumza na kusikiliza.** Watoto, hasa wale wanaogugumia huona kuzungumza kuwa raisi zaidi wakati kuna katizo chache na wanaona umakini wa wasikilizaji
- 6 Tazama jinsi una vyoingiliana na mtoto wako.** Jaribu kuongeza nyakati hizo zinazompa mtoto wako ujumbe kuwa kupunguza ukosoaji, mienendo ya usemi wa haraka, katizo na maswali.
- 7 Zaidi ya yote, onyesha kwamba unamkubali mtoto wako jinsi alivyo.** Tendo lenye nguvu zaidi litakuwa kumuunga mkono, iwe anagugumia au la.

### Kiingereza toleo kuchapishwa na:

Stuttering Foundation of America  
P.O. Box 11749  
Memphis, TN 38111-0749 , USA

### Mfasiri:

AFRICAN STUTTERING RESEACH CENTRE  
P.O. BOX 2379 Kigali  
RWANDA